TANGAZO LA SERIKALI NA. 76 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA,
(SURA YA 425)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 20(1)(d))*

KANUNI ZA USTAWI, MWENENDO NA NIDHAMU YA WANAFUNZI ZA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 619 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ustawi, Mwenendo na Nidhamu ya Wanafunzi za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ustawi, Mwenendo na Nidhamu ya Wanafunzi za Mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6 (1), kwa kuongeza neno “nje ya Shule” mara baada ya neno “mkutano”.

Marekebisho ya kanuni ya 7

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 7 (1), kwa kuongeza maneno “ndani au” mara baada ya neno “kusafiri”.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa-

(a) kuongeza neno “na Fidia inayolingana na uharibifu uliofanyika” mara baada ya maneno “Onyo kali” yanayoonekana katika safu ya tatu, kipengele cha 5;

(b) kuongeza neno “Mifumo ya TEHAMA” mara baada ya neno “alama” linaonekana katika kipengele cha 34 cha safu ya pili; na

(c) kufuta neno “inayopitishwa kwenye mifumo ya Tehama” yanayoonekana katika kipengele cha 34 cha safu ya pili, na badala yake kuweka maneno “ya mawasiliano”.

Marekebisho ya Jedwali la Pili

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Pili kwa kuongeza mara baada ya namba 3 inayoonekana kabla ya Jedwali, namba ifuatayo;

"4. Mwanafunzi atakayekiuka kanuni za mavazi hataruhusiwa kuingia Shuleni mpaka atakapovaa mavazi yanayokubalika kwa mujibu wa kanuni za Shule".

Dar es Salaam,
4 Januari, 2025

SAMWEL M. MANENO
*Mwenyekiti wa Bodi*